ISSN 0856-6976

# MUHTASARI WA TAMKO LA SERA YA FEDHA

# 2018/19

GAVANA
BENKI KUU YA TANZANIA

Juni 2018

**ISSN 0856-6976**

# MUHTASARI WA TAMKO LA SERA YA FEDHA

# 2018/19

**GAVANA**

**BENKI KUU YA TANZANIA**

Juni 2018

# Utangulizi

Kwa mujibu wa Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania ya mwaka 2006, Benki Kuu inatoa Tamko la Sera ya Fedha linaloweka bayana mwelekeo wa sera ya fedha kwa mwaka 2018/19. Tamko hili linajumuisha mapitio ya mwenendo wa uchumi na utekelezaji wa sera ya fedha ya mwaka 2017/18 na kuainisha malengo ya sera ya fedha kwa mwaka 2018/19 yanayoendana na malengo ya Serikali ya maendeleo ya kiuchumi. Tamko hili pia linaelezea hatua zinazokusudiwa kuchukuliwa ili kufikia malengo hayo.

## Mwenendo wa Uchumi wa Dunia

Kasi ya ukuaji wa uchumi wa dunia inakadiriwa kuwa iliongezeka kufikia asilimia 3.8 kwa mwaka 2017 ikilinganishwa na asilimia 3.2 mwaka 2016, ikichangiwa kwa kiasi kikubwa na ukuaji wa uchumi kwenye mataifa yanayoibukia kiuchumi na yale yanayoendelea. Ukuaji wa uchumi katika mataifa yaliyoendelea kiuchumi ulikuwa asilimia 2.3 mwaka 2017, ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 1.7 mwaka 2016. Ukuaji huo ulichochewa na shughuli za viwanda na huduma pamoja na mazingira bora ya sekta ya fedha. Katika mataifa yanayoibukia kiuchumi na yale yanayoendelea, kasi ya ukuaji wa uchumi ilikuwa ni asilimia 4.8 mwaka 2017 ikilinganishwa na asilimia 4.4 mwaka 2016. Ukuaji huo ulichochewa na kuongezeka kwa bei za bidhaa katika soko la dunia. Kasi ya ukuaji wa uchumi Kusini mwa jangwa la Sahara iliongezeka maradufu na kufikia asilimia 2.8, ikilinganishwa na asilimia 1.4 mwaka 2016 kutokana na kuongezeka kwa bei za bidhaa kwenye soko la dunia na uwekezaji katika miundombinu.

Kasi ya ukuaji wa uchumi wa dunia inatarajiwa kuongezeka zaidi kufikia asilimia 3.9 kwa mwaka 2018 na 2019 ukichochewa na matarajio ya kuongezeka kwa matumizi ya walaji, kuimarika kwa uwekezaji, pamoja na kuongezeka kwa shughuli za viwanda na biashara. Katika mataifa yaliyoendelea kiuchumi ukuaji wa uchumi unatarajiwa kufikia asilimia 2.5 mwaka 2018 kutoka asilimia 2.3 mwaka 2017 na baadaye kupungua hadi asilimia 2.2 mwaka 2019 kutokana na matarajio ya ukuaji mdogo wa uchumi wa Japan, Marekani, na eneo la Ulaya linalotumia sarafu ya Euro. Matarajio ya kupungua kwa kasi ya ukuaji wa uchumi kuelekea mwaka 2019 yanatokana na kuongezeka kwa mabadiliko ya sera ya mara kwa mara, hususan uwezekano wa kuongezeka kwa vikwazo vya kibiashara nchini Marekani. Kasi ya ukuaji wa uchumi katika mataifa yanayoibukia kiuchumi na yanayoendelea inatarajiwa kuimarika kutoka asilimia 4.8 mwaka 2017 hadi asilimia 4.9 mwaka 2018 na asilimia 5.1 mwaka 2019 ikichangiwa na kuongezeka kwa bei za bidhaa na uwekezaji katika miradi ya miundombinu.

Katika kipindi cha Julai 2017 hadi Aprili 2018, kasi ya mfumuko wa bei katika nchi zilizoendelea na zile zinazoibukia kiuchumi ulipungua isipokua nchini Marekani, India na Saudi Arabia. Katika eneo la Ulaya linalotumia sarafu ya Euro, mfumuko wa bei ulipungua kutokana na kushuka kwa bei za huduma na bidhaa zisizokuwa za nishati, wakati nchini Uingereza mfumuko wa bei ulishuka kutokana na kupungua kwa hali ya wasiwasi kuhusu Uingereza kujitoa katika Umoja wa Ulaya. Kupungua kwa mfumuko wa bei nchini China kulisababishwa na kupungua kwa bei za chakula. Katika ukanda wa Afrika ya Mashariki, wastani wa mfumuko wa

bei ulipungua kutokana na kushuka kwa bei za vyakula kulikosababishwa na kuongezeka kwa uzalishaji. Aidha, mfumuko wa bei nchini Marekani na Saudi Arabia uliongezeka kutokana na kupanda kwa bei ya nishati, wakati mfumuko wa bei nchini India ulisababishwa na kuongezeka kwa bei za huduma za jamii na nishati.

## Mwenendo wa Uchumi wa Tanzania

### *Tanzania Bara*

Uchumi umeendelea kuimarika ambapo kwa miaka ya karibuni Pato la Taifa limekua kwa wastani wa asilimia 7.1 kati ya mwaka 2013 na 2017. Katika mwaka 2017, uchumi ulikua kwa asilimia 7.1 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 7.0 mwaka 2016. Kiwango hiki cha ukuaji wa uchumi kimechochewa na kuendelea kuongezeka na kuimarika kwa miundombinu, kutengemaa kwa upatikanaji wa nishati na hali nzuri ya hewa. Kasi kubwa ya ukuaji wa uchumi ilishuhudiwa katika sekta ya uchimbaji madini, mawe na kokoto; usambazaji maji, uchukuzi na uhifadhi; habari na mawasiliano na ujenzi. Mchango mkubwa wa ukuaji wa uchumi ulitokana na shughuli za ujenzi (asilimia 22.7), uchukuzi na uhifadhi (15.6), kilimo (10.5), habari na mawasiliano (9.8). Mfumuko wa bei uliendelea kupungua kutokana na kuimarika kwa uzalishaji na upatikanaji wa chakula, kuimarika kwa upatikanaji wa nishati na uwepo wa sera thabiti za fedha na za kibajeti.

Katika kipindi cha Julai 2017 hadi Aprili 2018, mfumuko wa bei uliendelea kupungua na kufika wastani wa asilimia 4.5 ikilinganishwa na asilimia 5.2 katika kipindi kama hicho mwaka 2016/17. Mfumuko wa bei usiojumuisha bei za vyakula na nishati (*core inflation*) ulipungua na kufikia wastani wa

asilimia 1.6 ikilinganishwa na asilimia 2.4 kwa kipindi kama hicho mwaka 2016/17. Wakati huo huo, mfumuko wa bei unaojumuisha nishati (*energy inflation*) uliongezeka na kufikia wastani wa asilimia 11.8 ikilinganishwa na asilimia 9.3 katika kipindi kama hicho mwaka 2016/17 kutokana na kuongezeka kwa bei za mafuta katika soko la dunia.

Katika kipindi cha Julai 2017 hadi Aprili 2018, mapato ya Serikali yaliyokusanywa na kuwekwa kwenye akaunti zake zilizoko Benki Kuu ya Tanzania yameendelea kuongezeka na kufikia shilingi bilioni 14,204.5, sawa na ongezeko la asilimia 8.5 ikilinganishwa na kipindi kama hicho kwa mwaka wa fedha 2016/17. Ongezeko hili la makusanyo limetokana na kuongezeka kwa jitihada za Mamlaka ya Mapato Tanzania. Jumla ya matumizi yaliyolipiwa kutoka kwenye akaunti za Serikali zilizoko Benki Kuu yalifikia shilingi bilioni 15,625.4; ambapo matumizi ya kawaida yalikuwa shilingi bilioni 11,631.5 sawa na ongezeko la asilimia 7, na matumizi ya maendeleo yalikuwa shilingi bilioni 3,993.9 sawa na ongezeko la asilimia 13.5, ikilinganishwa na kipindi kama hicho mwaka 2016/17.

Katika kipindi cha Julai 2017 hadi Aprili 2018, urari kwenye mizania ya malipo (*overall balance of payments*) ulikuwa na ziada ya dola za Kimarekani milioni 299.2 ikilinganishwa na dola za Kimarekani milioni 591.7 katika kipindi kama hicho mwaka 2016/17. Hali hii ilisababishwa na kuongezeka kwa thamani ya bidhaa zilizoagizwa kutoka nje ya nchi. Akiba ya fedha za kigeni ilikuwa dola za Marekani milioni 5,251.1 mwishoni mwa mwezi Aprili 2018, ambayo inatosheleza kuagiza bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi cha takriban miezi 5.4, ukiondoa bidhaa na huduma zinazogharamiwa na uwekezaji kutoka nje. Mauzo ya huduma nje ya nchi yalifikia dola za Kimarekani milioni 3,437.5 katika kipindi

cha mwezi Julai 2017 hadi Aprili 2018 ikilinganishwa na mauzo ya dola za Kimarekani 3,123.5 katika kipindi kama hicho mwaka 2016/17. Ongezeko hilo lilitokana na kuongezeka kwa mapato ya utalii, usafirishaji na uchukuzi. Mapato ya utalii yaliongezeka kwa asilimia 15.0 yakitokana na kuongezeka idadi ya watalii ikiwa ni matokeo ya jitihada za Serikali na Sekta binafsi kuvutia utalii. Vilevile, mapato ya usafirishaji yaliongezeka kwa asilimia 9.7 kutokana na kuongezeka kwa usafirishaji wa mizigo ya kimataifa (*transit goods*) baada ya kuondolewa kwa kodi ya ongezeko la thamani (VAT) kwa huduma za mizigo ya aina hiyo na kuboreshwa kwa huduma katika bandari ya Dar es Salaam hususan kuimarishwa kwa usalama wa mizigo. Wakati huo huo, thamani ya malipo ya huduma nje ya nchi (*services payment*) ilikuwa dola za Kimarekani milioni 1,822.0 sawa na ongezeko la asilimia 6.4 yakiwa yametokana na kuongezeka kwa huduma za kibiashara.

Deni la nje liliongezeka kwa dola za Marekani milioni 1,376.5 hadi kufikia dola za Marekani milioni 20,027.6 mwishoni mwa mwezi Aprili 2018, ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 18,651.1 mwezi Juni 2017, ambapo asilimia 78.4 ya deni hilo lilikuwa ni deni la Serikali na taasisi za umma. Katika kipindi kama hicho mwaka 2016/17, deni la nje liliongezeka kwa dola za Marekani milioni 535.3 hadi kufikia dola za Marekani milioni 17,758.1 mwishoni mwa mwezi Aprili 2017. Ongezeko la deni la nje katika kipindi cha mwezi Julai 2017 hadi Aprili 2018 limetokana na mikopo mipya pamoja na malimbikizo ya riba (*interest arrears*). Pamoja na deni hilo kuongezeka bado ni himilivu. Matokeo ya tathmini ya uhimilivu wa deni la nje la Taifa yanaonesha kuwa thamani halisi ya deni la nje ikilinganishwa na Pato halisi la Taifa ni asilimia 19.7, ambayo ni chini ya

ukomo uliowekwa kimataifa wa kiwango cha uhimilivu wa deni la nje cha asilimia 40.0. Deni la ndani liliongezeka na kufikia shilingi bilioni 12,739.1 mwishoni mwa mwezi Aprili 2018 kutoka shilingi bilioni 11,788.8 mwezi Juni 2017. Ongezeko hilo lilitokana na Serikali kukopa kupitia dhamana za Serikali kwa ajili ya kugharamia bajeti ya Serikali kwa mwaka 2017/18. Katika kipindi kama hicho mwaka 2016/17, deni la ndani liliongezeka na kufikia shilingi bilioni 11,132.3 kutoka shilingi bilioni 10,038.4.

Katika mwaka ulioishia mwezi Aprili 2018, sekta ya kibenki imeendelea kukua. Rasilimali za sekta ya benki zilikua kwa asilimia 5.6 na kufikia shilingi bilioni 29,877.3 mwishoni mwa mwezi Aprili 2018. Kiujumla, pamoja na kuwepo kwa mikopo chechefu, sekta ya kibenki imeendelea kuwa imara, salama na yenye kutengeneza faida, ikiwa na mitaji na ukwasi wa kutosha zaidi ya kiwango kinachotakiwa kisheria. Benki Kuu imeendelea kusimamia utekelezaji wa hatua za kuimarisha udhibiti wa vihatarishi katika sekta ya fedha (*risk management practices*) kwa kupitia upya kanuni na miongozo ili iendane na mabadiliko ya sasa. Pia, Benki Kuu imeziagiza benki zote kutekeleza mikakati ya kuboresha utoaji, usimamizi na ulipaji mikopo, ikiwa ni pamoja na kuzitaka benki kutumia kwa lazima taarifa ya historia za wakopaji kabla ya kutoa mkopo (*mandatory use of credit reference bureau reports*).

Katika mwezi Januari 2018, Benki Kuu ilisitisha leseni za benki za biashara zilizokuwa na mitaji pungufu chini ya kiwango kilichowekwa kisheria baada ya kushindwa kutimiza matakwa hayo ndani ya muda wa miaka mitano. Benki hizo ni Covenant Bank for Women (Tanzania) Limited, Efatha Bank Limited, Njombe Community Bank Limited, Kagera Farmers' Cooperative Bank Limited, na Meru Community Bank Limited. Aidha,

mwezi Mei 2018, wamiliki wa Benki ya Twiga walikamilisha utaratibu wa kuiunganisha na Benki ya TPB. Pia, Benki ya Dunia kwa kushirikiana na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) walifanya tathmini ya sekta ya fedha, ili kubaini changamoto zilizopo katika sekta hiyo na kutoa ushauri wa jinsi ya kukabiliana na changamoto hizo. Tathmini ya awali inaonyesha kwamba sekta ya fedha ni tulivu.

Ili kuhakikisha usalama na ufanisi wa mifumo ya malipo ya kitaifa, Benki Kuu imeendelea kuimarisha mfumo wa usimamizi na utoaji leseni kwa watoa huduma wapya wa mifumo ya malipo. Katika mwaka 2017/18 mifumo ya malipo imeendelea kufanya kazi kwa ufanisi na kumekuwepo na ukuaji wa miamala ikiwa ni matokeo ya ongezeko la matumizi ya mifumo ya kidijitali kama mfumo wa kuhamisha fedha kielektroniki (*Electronic Fund Transfers -EFT*) kupitia mfumo wa kubadilishana hundi (*Tanzania Automated Clearing System -TACH*), mfumo wa malipo kati ya mabenki (*Tanzania Interbank Settlement System -TISS*) na mfumo wa malipo wa Afrika Mashariki (*East Africa Payment System -EAPS*).

***Zanzibar***

Katika mwaka 2017, uchumi wa Zanzibar ulikua kwa asilimia 7.5, ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 6.8 mwaka 2016. Ukuaji huo ulichangiwa zaidi na huduma za malazi na chakula (asilimia 36) kilimo, misitu na uvuvi (asilimia 22.7) na viwanda (asilimia 13.3). Mfumuko wa bei ulipungua hadi asilimia 2.6 mwezi Aprili 2018 ikilinganishwa na asilimia 5.4 mwezi Juni 2017. Hali hiyo ilitokana na kupungua kwa mfumuko wa bei za vyakula kutoka asilimia 4.6 mwezi Juni 2017 hadi

asilimia hasi 1.1 mwezi Aprili 2018 ikiwa ni matokeo ya kupungua kwa bei za unga wa mahindi, ndizi na sukari.

Katika kipindi cha Julai 2017 hadi Aprili 2018, jumla ya mapato ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar yalifikia shilingi bilioni 745.9. Mapato ya ndani yalikuwa shilingi bilioni 572.0, na mapato ya nje yalikuwa shillingi bilioni 31.1. Makusanyo ya ndani yalifika asilimia 100.1 ya lengo ambapo makusanyo ya kodi yalifikia asilimia 99.6 na makusanyo yasiyo ya kodi yalifikia asilimia 105.0 ya lengo. Makusanyo mazuri ya mapato yalitokana na jitihada za mamlamka za mapato na kuongezeka kwa uwajibikaji wa walipakodi. Jumla ya matumizi ya Serikali ilikuwa shilingi bilioni 746.5; kati ya hizo, matumizi ya kawaida yalikuwa ni shilingi bilioni 517.0, wakati matumizi ya maendeleo yalikuwa ni shilingi bilioni 229.4.

Katika kipindi cha Julai 2017 hadi Aprili 2018, urari wa biashara ya bidhaa, huduma na uhamisho wa mali nje ya nchi uliimarika na kufikia ziada ya dola za Kimarekani milioni 33.1 ikilinganishwa na ziada ya dola za Kimarekani milioni 29.1 katika kipindi kama hicho mwaka 2016/17. Ongezeko hilo la ziada lilichangiwa na mauzo ya karafuu na huduma za utalii na uhamisho wa mali (*current transfers*). Vilevile, thamani ya mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi iliongezeka kufikia dola za Kimarekani milioni 213.5 kutoka dola za Kimarekani milioni 152.2 katika kipindi kama hicho mwaka 2016/17. Aidha, thamani ya bidhaa na huduma zilizonunuliwa kutoka nje iliongezeka kwa asilimia 46.5 na kufikia dola za Kimarekani milioni 216.4 kutokana na uagizaji wa mashine na vyombo vya usafiri, bidhaa zinazotumika katika uzalishaji (*intermediate goods*) na bidhaa za chakula hususan ngano, mchele na sukari.

## Utekelezaji wa Malengo ya Sera ya Fedha ya Mwaka 2017/18

### *Malengo ya Sera ya Fedha*

Benki Kuu ya Tanzania iliendelea kuhakikisha kuwa kuna ukwasi wa kutosha katika uchumi unaoendana na malengo ya uchumi mpana hususan utulivu wa bei na ukuaji mkubwa wa uchumi pamoja na utulivu wa masoko ya fedha na riba. Malengo ya sera ya fedha ya mwaka 2017/18 yalitathiminiwa upya wakati wa mapitio ya nusu mwaka yaliyofanyika mwezi Februari 2018 ili kuzingatia matokeo ya maendeleo kwenye uchumi mpana. Katika mwaka 2017/18, Benki Kuu ililenga kutekeleza sera ya fedha yenye malengo yafuatayo:

i. Ukuaji wa wastani wa fedha taslim usiozidi asilimia 10.7;

ii. Ukuaji wa ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) usiozidi asilimia 12.0;

iii. Ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi usiozidi asilimia 11.5; na

iv. Kuwa na akiba ya fedha za kigeni inayotosha kuagiza bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi kisichopungua miezi minne (4.0).

### *Utekelezaji wa Sera ya Fedha*

Katika kipindi cha Julai 2017 hadi Aprili 2018, Benki Kuu iliendeleza sera ya kuongeza ukwasi kwenye uchumi (*accommodative monetary policy*) iliyoanza kutekelezwa nusu ya pili ya mwaka 2016/17. Sera hii ilitekelezwa ili kuchochea utoaji wa mikopo kwa sekta binafsi ambayo ilikuwa katika kiwango cha chini ili kusaidia kuendeleza shughuli mbalimbali za kiuchumi.

Utekelezaji wa Sera ya fedha katika kipindi hiki ulikusudia kuongeza utulivu wa riba ya siku moja baina ya mabenki (*overnight interbank cash market rate*) kwa kufuatilia na kudhibiti kiwango cha amana za benki za biashara zilizopo Benki Kuu (*clearing balances*) ili ziendane na mahitaji ya msimu. Katika kipindi hiki, Benki Kuu ilishusha riba yake (*discount rate*) na kufikia asilimia 9 kutoka asilimia 12 mwezi Agosti 2017 na kuendelea kuongeza ukwasi katika uchumi kupitia ununuzi wa fedha za kigeni katika masoko ya ndani, kubadilishana fedha za kigeni (*foreign exchange swaps*) na kununua dhamana za muda mfupi kutoka benki za biashara (*reverse repo*). Vilevile Benki Kuu iliendelea kutoa mikopo ya muda mbalimbali kwa Benki za biashara (*Lombard, intraday loans and discount window*) ili kukidhi mahitaji ya muda mfupi ya ukwasi huku ikihakikisha kuwa ukwasi unaozidi unaondolewa kupitia mauzo ya dhamana za muda mfupi (*repos*).

Hatua zote hizi zilizochukuliwa na Benki Kuu ziliboresha hali ya ukwasi katika masoko ya fedha na kushusha riba ya siku moja baina ya mabenki iliyopungua na kufikia wastani wa asilimia 1.29 mwezi Aprili 2018 ikilinganishwa na asilimia 4.08 mwezi Juni 2017 na asilimia 7.19 mwezi Aprili 2017. Vilevile riba za dhamana za muda mfupi za Serikali (*Treasury Bills*) zilipungua hadi kufikia wastani wa asilimia 4.04 mwezi Aprili 2018 ikilinganishwa na asilimia 13.51 mwezi Aprili 2017. Pamoja na kwamba hatua zilizochukuliwa na Benki Kuu zilisaidia kushusha riba kwenye masoko ya fedha, riba za mikopo ya benki za biashara kwa sekta binafsi zimeendelea kuwa juu huku riba za amana zikipungua. Kuongezeka kwa riba za mikopo kwa sekta binafsi kumetokana na benki hizo kuweka tahadhari kubwa kwa wateja (*risk premium*) hali inayochangiwa zaidi na kuwepo kwa kiwango kikubwa cha mikopo chechefu.

Kutokana na utekelezaji wa sera ya kuongeza ukwasi kwenye uchumi, ukuaji wa ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (*extended broad money supply*) uliongezeka hadi kufikia asilimia 7.0 mwezi Aprili 2018 ikilinganishwa na asilimia 6.0 mwezi Juni 2017. Vilevile, ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi umeanza kukua polepole na kufikia asilimia 0.7 mwezi Aprili 2018 ikilinganishwa na ukuaji hasi kwa miezi miwili ya Septemba na Oktoba 2017. Ukuaji wa ujazi wa fedha unategemewa kuimarika kutokana na kuendelea kutekeleza sera ya fedha inayoongeza ukwasi katika uchumi. Katika kipindi cha Julai 2017 hadi Aprili 2018 thamani ya shilingi ya Tanzania imeendelea kuwa tulivu pamoja na mabadiliko madogo yaliyotokea mwezi Aprili 2018 ambao huwa ni msimu wa mauzo kidogo ya bidhaa nje ya nchi na utalii.

**Matarajio ya Uchumi na Malengo ya Sera ya Fedha ya Mwaka 2018/19**

Katika mwaka 2018/19, Serikali zitaendelea kutekeleza Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano (*Second Five Year Development Plan, FYDP II 2016/17 – 2020/21*) pamoja na Mpango wa Kukuza Uchumi Zanzibar (*MKUZA III 2015-20*) inayolenga kuendeleza jitihada za kuweka misingi imara ya uendelezaji wa viwanda na kukuza uchumi. Malengo ya Serikali kwa mwaka 2018/19 ni:

i. Ukuaji wa Pato la Taifa wa asilimia 7.2 mwaka 2018;

ii. Mfumuko wa bei ulio ndani ya kiwango cha tarakimu moja; na

iii. Nakisi ya bajeti ya serikali ikijumuisha misaada kutoka nje (*including grants*) pamoja na malipo ya malimbikizo (*including clearence of arreas*) ya asilimia 3.2 ya Pato la Taifa mwaka 2018/19.

Kwa upande wa Zanzibar, Pato la Taifa linatarajiwa kukua kwa asilimia 7.2 mwaka 2018, wakati nakisi ya bajeti ya serikali ya Zanzibar inatarajiwa kuwa asilimia 3.8 ya Pato la Taifa mwaka 2018/19.

Ili kufikia malengo ya Serikali ya uchumi mpana kwa mwaka 2018/19, Benki Kuu ya Tanzania itaendelea kutekeleza sera ya fedha inayolenga kuimarisha utulivu wa bei pamoja na utulivu wa riba katika masoko ya fedha. Kwa mwaka 2018/19, Benki Kuu imepanga kufikia malengo yafuatayo:

i. Ukuaji wa wastani wa fedha taslim usiozidi asilimia 11.5;

ii. Ukuaji wa ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) usiozidi asilimia 12.2;

iii. Ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi usiozidi asilimia 10.2; na

iv. Kuwa na akiba ya fedha za kigeni inayotosha kuagiza bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi kisichopungua miezi minne.

Benki Kuu itaendelea kuhakikisha hali ya ukwasi inaendelea kuwa ya kuridhisha ili kusaidia ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi kulingana na mahitaji halisi ya uchumi. Katika kulisimamia jukumu hili, Benki Kuu itaendelea kutumia nyenzo za sera ya fedha ili kuhakikisha kuwa kiasi cha ukwasi kwenye benki za biashara kinabakia katika kiwango kinachoendana na mahitaji ya wakati huo, na hivyo kuleta utulivu wa riba katika soko la fedha baina ya mabenki. Aidha, katika kuboresha uendeshaji wa soko la fedha baina ya benki za biashara na kufanya soko hilo kuwa la kisasa

zaidi, Benki Kuu imerekebisha na kuboresha mfumo wa dhamana kwa kuongeza wigo wa dhamana za Serikali zinazokubalika kisheria kukopea kutoka Benki kuu ambapo dhamana zote za serikali zinakubalika. Vilevile, Benki Kuu imetengeneza mfumo wa kielektroniki utakaotumiwa na benki za biashara katika kukopeshana (*electronic interbank market trading platform*) ili kuongeza uwazi wa soko hilo la fedha. Benki Kuu pia imeandaa kanuni za uendeshaji wa soko la fedha baina ya mabenki, pamoja na makubaliano ya uendeshaji ya soko la mikopo ya muda mfupi (*General Master Repurchase Agreement – GMRA*). Hatua hizi zitaboresha upatikanaji wa ukwasi baina ya benki za biashara na kuongeza uwazi kwenye soko la fedha, hali ambayo itaendela kuimarisha mwenendo na utulivu wa viwango vya riba katika soko la fedha.

Katika mwaka 2018/19, Benki Kuu inakusudia kuanza kutekeleza sera ya fedha chini ya mfumo mpya unaotumia riba ya Benki Kuu (*Central Bank Rate*), ili kuongeza ufanisi wa sera ya fedha katika kufikia malengo ya utulivu wa bei na ukuaji wa uchumi. Chini ya mfumo huu, Benki Kuu itatumia mwenendo wa riba za muda mfupi (*interbank cash market interest rate*) kama kiashiria cha msingi cha hali ya ukwasi badala ya ujazi wa fedha taslimu (*reserve money*).

## Matarajio na Hitimisho

Uchumi wa Tanzania unatarajia kuendelea kuwa imara katika mwaka 2018/19 kutokana na Serikali kuendelea na utekelezaji wa awamu ya Pili ya Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (*Second Five Year Development Plan, FYDP II 2016/17 – 2020/21*) na Mpango wa Kukuza

Uchumi Zanzibar (*MKUZA III 2015-20*), pamoja na hali nzuri ya hewa, kuimarika kwa mazingara ya kufanya biashara na matarajio ya kuimarika kwa uchumi wa dunia. Pamoja na kwamba Jumuiya ya nchi zinazouza mafuta duniani (OPEC) imeendelea kutekeleza hatua za kupunguza uzalishaji wa mafuta, mfumuko wa bei unatarajiwa kubakia ndani ya tarakimu moja katika mwaka 2018/19 na karibu ya lengo la muda wa kati la asilimia 5. Matarajio haya yanatokana na mwelekeo wa kuimarika kwa uzalishaji wa chakula kwa sababu ya hali nzuri ya hewa pamoja na upatikanaji wa mbolea na kuimarika upatikanaji wa nishati.

Aidha, Benki Kuu itaendelea kutekeleza sera thabiti ya fedha ili kuendeleza utulivu katika uchumi mpana na kwa kuzingatia uwezekano wa kuongezeka kwa mfumuko wa bei unaotokana na mitikisiko katika uzalishaji *(supply shocks*). Benki Kuu ipo katika hatua za juu za kuanza kutumia mfumo mpya wa sera ya fedha unaolenga riba ili kuimarisha ufanisi katika kufikia malengo ya utulivu wa bei na ukuaji wa uchumi. Chini ya mfumo huu, sera ya fedha itahakikisha kuwa riba baina ya mabenki (*interbank cash market rate*) inaendana na riba ya Benki Kuu *(BOT policy rate*) itakayoamuliwa na Kamati ya Sera ya Fedha (*Monetary Policy Committee*).

Benki Kuu itaendelea kufuatilia vihatarishi katika mwenendo mzima wa uchumi wa nchi na wa dunia katika kufikia lengo la utulivu wa bei na kuchukua hatua muafaka na zenye kuzingatia uwiano na sera za kibajeti. Kulingana na tathmini ya mwelekeo wa uchumi wa dunia na uchumi wa Tanzania, pamoja na sera zinazotarajiwa kutekelezwa, Benki Kuu inaamini kuwa malengo yaliyowekwa katika Sera ya Fedha kwa mwaka 2018/19 yatafikiwa.

Kwa maelezo zaidi wasiliana na:
Mkurugenzi wa Utafiti na Sera za Uchumi
Benki Kuu ya Tanzania, 2 Mtaa wa Mirambo, 11884 Dar es Salaam
Simu: +255 22 2233328, +255 22 2233350, Nukushi: +255 22 2234060
Tovuti: http://www.bot.go.tz

Kimepigwa Chapa na Identity Promotion Ltd